# MAONESHO YA NANENANE 2026

(HABARI ZOTE NA FRED ALFRED, DODOMA)

**BILIONI 700/=>> Fedha zilizotolewa na Benki ya TADB kufadhili miradi ya kimkakati**

## BRELA yaboresha mfumo wa usajili

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), umebainisha kuwa, umefanya maboresho makubwa katika mfumo wake wa usajili ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Akizungumza katika maonesho hayo, Ofisa Usajili wa BRELA, Yusuf Mwasakafika, alisema wananchi wanaweza kupata huduma mbalimbali, ukiwemo usajili wa majina ya biashara, usajili wa kampuni, utoaji wa leseni za biashara 'Kundi A' na huduma zinazohusiana na usajili wa alama za biashara na viwanda.

Alisema uwepo wa BRELA katika maonesho hayo, unalenga kuwahamasisha wakulima wanaofanya kilimo cha kibiashara na kurasimisha shughuli zao ili wajiamini zaidi kufanya biashara na kufikia masoko.

"Tunawahamasisha wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla wanaofanya shughuli mbalimbali za kilimo, kufika hapa na kupata huduma ambazo wangeweza kuzitafuta wakiwa ofisini, lakini sasa wanazipata hapa," alisema Mwasakafika.

Vilevile, alisema BRELA inatumia maonesho hayo kutoa elimu kuhusu mfumo mpya wa usajili ulioboreshwa, ambao umefanyiwa maboresho kurahisisha upatikanaji wa huduma na kupunguza changamoto ambazo baadhi ya wafanyabiashara, walikuwa wakikumbana nazo.

Kwa mujibu wa Mwasakafika, kupitia mfumo huo mpya, baadhi ya huduma zinafanyika kwa njia ya mtandao bila mhusika kulazimika kufika moja kwa moja katika ofisi za BRELA.

> **Tunawahamasisha wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla wanaofanya shughuli mbalimbali za kilimo, kufika hapa na kupata huduma...**
>
> Ofisa Usajili wa BRELA, Yusuf Mwasakafika.

Alisema miongoni mwa maboresho yaliyofanyika ni kuwezesha uwasilishaji nyaraka mbalimbali kwa njia ya mfumo, zikiwemo nyaraka zinazohusiana na madeni yanayohitaji kuwasilishwa katika usajili.

"Kwa kutumia mfumo huu, sasa tumeboresha huduma kiasi kwamba mtu anaweza kuwasilisha nyaraka akiwa nyumbani kwake au benki, bila kulazimika kufika BRELA," amesema.

Hata hivyo, aliwasisitiza wananchi wanaotaka kutumia mfumo huo kuhakikisha wanakuwa na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), namba ya simu inayotumika pamoja na anuani sahihi ya barua pepe, ambazo ni muhimu katika kupata huduma kupitia mfumo.

# TADB yatoa bilioni 700/- kufadhili miradi kimkakati

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege, amesema benki hiyo, imetoa zaidi ya sh. bilioni 700 kufadhili miradi ya kimkakati.

Amesema fedha hizo, zimetolewa kufadhili miradi ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini, huku vyama vya ushirika vinavyozalisha kahawa, hususan katika mikoa ya Kagera na Kigoma, vikiwa miongoni mwa wanufaika wakubwa wa huduma za fedha zinazotolewa na benki hiyo.

Nyabundege aliyasema hayo jijini hapa jana katika Viwanja vya Maonesho ya Wakulima Nanenane.

Pia, alisema TADB imewezesha mradi wa kisasa wa uzalishaji na uchakataji samaki uliopo Bagamoyo, unaotumia teknolojia ya kisasa iliyopatikana kutoka Misri, ambayo kwa sasa ina uwezo wa kuhifadhi hadi tani 90 za samaki kwa mwezi kwa kuzingatia viwango vya utunzaji mazingira.

Nyabundege alisema mradi huo, umefungua soko kubwa la samaki, umeongeza thamani ya mazao ya uvuvi na umeifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazotumia teknolojia hiyo ya kisasa katika sekta ya uvuvi.

"Tunaendelea kufanya vizuri katika kufadhili miradi yenye tija kwa uchumi wa nchi. Lengo letu ni kuhakikisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, zinakuwa nguzo kuu za maendeleo ya uchumi," amesema Nyabundege.

Kwa upande wake, mnufaika wa mradi wa samaki wa Bagamoyo, Simon Simalenga alisema ufadhili wa TADB, umewezesha matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kuhifadhi samaki, hatua iliyoongeza uzalishaji, kupunguza upotevu wa mazao na kufungua masoko mapya ya ndani na nje ya nchi.

Alisema uwezo wa kuhifadhi tani 90 za samaki kwa mwezi, umeongeza mapato ya biashara, umezalisha ajira kwa vijana na kuchangia kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje, hivyo kuokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza bidhaa zinazoweza kuzalishwa nchini.

**BIASHARA**




**WAFABIASHARA** ndogondogo 'machinga' wakiuza mito katika Barabara ya Bagamoyo, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, jana. (Picha na Emmanuel Ndege).

## e-GA yaendelea kurahisisha huduma za serikali kidijitali

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (e-GA), imeendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kidijitali kwa kuunda na kuendeleza mifumo mbalimbali inayorahisisha utoaji huduma za serikali, kuongeza uwazi na kuboresha ufanisi wa taasisi za umma.

Akizungumza katika Maonesho ya Wakulima Nanenane yanayoendelea jijini Dodoma, Meneja wa Mawasiliano wa e-GA, Subira Kaswaga, alisema lengo la mamlaka hiyo ni kuhakikisha kazi za serikali, zinafanyika kwa urahisi, haraka na ufanisi kupitia matumizi ya mifumo ya kidijitali.

Alisema e-GA imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Kilimo, kutengeneza mifumo mbalimbali ukiwemo wa e-Kilimo, unaowezesha ukusanyaji taarifa za wakulima, usimamizi wa taasisi zilizo chini ya wizara na utoaji wa vibali mbalimbali vinavyohusu sekta ya kilimo.

"e-GA imeshirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuanzisha mfumo wa kidijitali unaosimamia shughuli za vyama vya ushirika, ambapo wakulima wanaweza kufuatilia masoko ya mazao yao, kujua mauzo yanapofanyika na kupata taarifa mbalimbali zinazoongeza uwazi katika usimamizi wa vyama hivyo.

Alisema e-GA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imeunda Mfumo wa Usimamizi wa Mbolea (Fertilizer Information System - FIS) unaosimamia usajili wa wazalishaji na waagizaji wa mbolea kutoka ndani na nje ya nchi na kuwezesha ufuatiliaji wa bei ili wakulima wanufaike na mbolea kwa bei elekezi.

Kaswaga aliongeza kuwa, e-GA imefanikiwa kuunganisha taasisi mbalimbali za serikali kupitia mifumo ya kidijitali, hatua inayowezesha taasisi hizo kubadilishana taarifa haraka na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Dodoma na maeneo jirani, kutembelea banda la e-GA katika maonesho ya nanenane ili kujionea mifumo mbalimbali ya kidijitali inayotumika serikalini.

**Serikalini**

**MIFUMO**

Alisema e-GA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imeunda Mfumo wa Usimamizi wa Mbolea...